

KIDATO CHA PILI

MAAGIZO; jibu maswali yote.

Jina.....kidato.....

UFAHAMU

Soma kazi hii ya ufahamu kisha ujibu maswali yatakayofuata.

Biashara ni hali ya kuuza na kununua vitu mbalimbali. Utoaji wa huduma fulani kwa ajili ya malipo pia huchukuliwa kama shughuli ya biashara. Mfanyabiashara mzuri anafaa kuwa na sifa ya kuzungumza vizuri na kusikiliza maoni ya wateja wake. Pia anafaa ajue kuwa kila aina ya biashara ina uwezo wa kumfanikisha.

Mtu yeyote anapotaka kufanya biashara, ni vizuri ajiandae kifikira. Jambo hili litamwezesha kutambua uwezekano wa kupata faida au hasara. Iwapo mtu hana mtaji wa kutosha, inafaa atambue biashara ambazo zinahitaji mtaji mdogo. Kwa sababu ya mtaji mdogo, baadhi ya watu siku hizi wanawekeza katika biashara mbalimbali kama ; kuanzisha mikahawa, ufugaji wa kuku, huduma za kuendesha bodaboda au magari, biashara ya duka la rejareja, biashara ya mazao kama vile mahindi, maharagwe, mchele, mboga kama vile kabeji, nyanya, vitunguu, karoti, biringanya, sukumawiki na hata pia matunda kama maembe, nanasi, tikiti maji, parachichi na mengine. Saluni ndogo na miradi mingine mbalimbali. Kuna biashara pia za Sanaa ambazo hujumuisha uuzaji wa vitu mbalimbali vinavyotengenezwa kwa mikono.

Baadhi ya biashara pia ambazo zinahitaji mtaji mkubwa ni kama vile biashara kama za uuzaji wa magari na pikipiki, uuzaji wa pea za vyombo mbalimbali au kuanzisha shule na miradi mingine mikubwa. Aidha, ni muhimu kwa mjasiriamali yeyote kwanza kutambua vitu au huduma ambazo zinahitajika katika eeo fulani. Kwa hivyo, kila mtu anao uwezo wa kuanzisha biashara yeyote ile kulingana na uwezo wa mtaji alionao.

MASWALI

- 1, Biashara ni nini?
- 2, Mfanyabiashara yeyote anafaa kufanya nini?
- 3, Pia anafaa kufanya nini?
- 4, Mtu yeyote anayetaka kufanya biashara ni vizuri afanye nini?
- 4, Iwapo mtu hana mtaji wa kutosha ni vizuri afanye nini?
- 5, Taja aina ya mboga zilizotajwa katika ufahamu.
- 6, Taja aina ya matunda yaliyotajwa katika ufahamu
- 7, Taja nafaka iliyotajwa katika ufahamu.
- 8, Biashara ambayo inahitaji mtaji mkubwa ni zipi?

2) INSHA

Katika jamii yako kuna aina mbalimbali ya biashara ambazo hufanyika. Kuna biashara ya kununua na kuuza kwa bidhaa na vitu vingine. Kuna biashara ya kuuzwa kwa bidhaa dukani, mahotelini, mikahawani, zahanati na pia sokoni. Mama yako amekupa shilingi elfu hamsini kununua vitu vya kutumia nyumbani.

Andika insha ukionyesha vitu utakavyo

nunua.....
.....
.....
.....
.....
.....

